



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS,
TAWALA ZA MIKOZA ZA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA KAHAMA**



Kumb.Na KMC/R/30/11/72

24 Machi, 2022

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama anapenda kuwatangazia Wananchi wote wenye sifa, nafasi Mia Nne na Thelathini (**430**) za Ajira ya Muda ya wakusanya Taarifa kwenye zoezi la Anuani za makazi katika Kata, Vijiji na Mitaa yote ya Halmashauri ya Manispaa Kahama.

SIFA ZA MWOMBADI

- i. Mwombaji awe Raia wa Tanzania.
- ii. Awe Mkazi wa Kijiji au Mtaa uliopo katika Manispaa ya Kahama.
- iii. Awe amehitimu Kidato cha Nne na kuendelea.
- iv. Awe anamiliki Simu janja *Android* yenye uwezo wa kukaa na chaji kwa siku nzima.
- v. Awe na barua pepe (email address) inayofanya kazi
- vi. Awe na uwezo wa kusoma Ramani za Mitaa na Vijiji.
- vii. Awe Mwadilifu na ambaye hajawahi kukutwa na hatia Mahakamani.
- viii. Awe na uwezo wa kufanya kazi kwa kujituma bila kusimamiwa.
- ix. Awe Mkazi wa Kata anapoombea nafasi hiyo ya Kazi.
- x. Awe na Umri wa kuanzia Miaka 18 hadi 35.

KAZI NA MAJUKUMU

- a.)Kugawa/kuandika Namba za Nyumba, Viwanja na maeneo ya huduma
- b.) Kukusanya taarifa za Nyumba, Viwanja na maeneo ya huduma.
- c.)Kukusanya taarifa za wamiliki wa Nyumba, Viwanja na Maeneo ya huduma kwa kutumia Mfumo wa Anuani za Makazi.
- d.)Kutuma Data kwenye Mfumo wa Anuani za Makazi.

MAOMBI YAAMBATANISHWE NA;

- i. Nakala ya Cheti cha Kidato cha Nne na kuendelea
- ii. Barua ya maombi ipitishwe na Mtendaji wa Kijiji au Mtaa anapoishi Mwombaji
- iii. Katika barua ya maombi, weka Namba yako ya simu inayopatikana muda wote.
- iv. Barua zibandikwe picha mbili (2) - Passport size.
- v. Waombaji watakaokidhi sifa na vigezo watajulishwa tarehe ya usaili.
- vi. Mwisho wa kupokea maombi ni **29/03/2022** saa **9:30** alasiri.
- vii. Maombi yote yaelekezwe Ofisi ya Mkurugenzi Manispaa ya Kahama kwa Anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi wa Manispaa,

Barabara ya Boma,

S.L.P 472,

KAHAMA

Limetolewa na:



C. B. Mkusa

**KAIMU MKURUGENZI WA MANISPAA
KAHAMA**

MUNICIPAL DIRECTOR
KAHAMA MUNICIPAL COUNCIL
P.O. Box 472
KAHAMA